

**MOMBASA COUNTY ASSEMBLY****HANSARD REPORT**Wednesday, 15<sup>th</sup> February, 2017

The House met at 2:45pm.

*(Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid) in the Chair)***PRAYERS****Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Members may sit down. Yes, Clerk.**NOTICE OF MOTION**

Hon Fadhili Fadhili Makarani...

**Hon. Mwalimu:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika nimesimama kuwasilisha notisi ya mswada tukielewa kuwa watumishi wa afya ya jamii wanaojulikana sana kama *CHW* ni kiungo muhimu katika jamii zetu na wanatoa mchango mkubwa katika kazi zao za kujitolea.

Itakua ni vyema kama serikali ya Kaunti kuwatunuku kwa njia moja ama nyengine Mheshimiwa Spika; pia tunaelewa kuwa hospitali za Kaunti ni haki kuwa zinatoza watu wote ada za huduma za afya hata watumishi hawa hawa wanaotumikia wananchi wetu wakienda kupata matibabu kutoka kwa Serikali hizi za Kaunti na tukizingatia kwa umakini wanalipishwa ada hizi za hospitali ilhali wamejitolea kutoa usaidizi wa kimatibabu bila malipo.

Mheshimiwa Spika nalihimiza Bunge hili kupitisha ya kuwa serikali ya Kaunti iwaruhusu watumishi wa afya ya jamii, hawa *CHW's* watibiwe kwanzo ikiwezekana bila malipo katika Spitali za Kaunti ama wapewe kiwango ambacho ni (??) wanachoweza kujimudu na kulingana na uzito wa jambo hili mimi naomba nipewe muda wa kama wiki mbili kwa sababu nimetuma maombi haya kwa muhusika wa afya ili aweze kunipa mipangilio yake pia maana ni jambo ambalo alivyonielea ni kuwa lina mambo ya bajeti ndani yake, nimepeleka uasilishi huu vile naomba kupitia kiti chako najua ina umuhimu lakini naomba kiti chako nikipewa kama wiki mbili.

Na pia vile vile niangalie Serikali zingine za Kaunti zinafanya namna gani; hini Mheshimiwa Spika ina umuhimu tuwaangalie wafanyi kazi hawa ama hawa *CHW's* ili tuweze kuwasaidia kama vile wao walivyojitolea kusaidia. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): *Sawa, Mheshimiwa Fadhili umeruhusiwa kufanya uchunguzi zaidi....kusubiri taarifa ya Mswada huu utakuja baada ya wiki mbili kama alivyoomba Mheshimiwa Fadhili, ahsante.*

Members of this House, we have Honourable Members from Embu County Assembly, Committee of Education they have visited our County today, they are our visitors and they are here on business.

I would like to appreciate the Honourable Members who are sitting up there, so I recognize their presence in front this House. With us is Hon Winrose Ireri, Chairperson...

*(Applause)*

Please stand so that the House can see you, thank you very much.

We have got Hon James Kathendu, Vice Chairperson...

*(Applause)*

We have Hon Steve Simba, Member...

*(Applause)*

We have Hon Shunem Gatitu, Member...

*(Applause)*

We have Hon Rose Ndwiga, Member...

(Applause)

We have Hon Patrick Rugendo, Member;

(Applause)

We have Hon Stephen Nzioka, Committee Clerk...

(Applause)

We have Hon Jacob Njeru, aide to Hon James...

(Applause)

Honourable Members from Embu County you are welcomed to Mombasa County, thank you.

(Honorable Members from Embu County Assembly bowed)

Yes, Clerk.

### STATEMENTS

Hon. Amir Thoya.

**Hon. Thoya:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika kwa ruhsa yako na ruhsa ya Bunge letu tukufu, nimesimama kama Mwenyekiti wa Kamati ya kazi za umma, uchukuzi na miundo msingi.

Mheshimiwa Spika napenda kutoa taarifa ifuatayo kufuatia uchafuzi wa mazingira katika eneo la Changamwe, hasa hasa kama ilivyo weza kuombwa na Wwakilishi wa wodi ya Changamwe Mheshimiwa Jimmy Odari katika kikao cha kumi na sita, Alhamisi tarehe tisa mwezi wa pili mwaka 2017 pamoja kama ujenzi wa barabara unavyoendelea kule Changamwe.

Mheshimiwa Spika Kamati ya uchukuzi na miundo msingi iliweza kufanya mkutano na mkuu wa *Kenya National Highway Authority (KENHA)*, Eng. Makori siku ya Jumanne tarehe 14 mwezi wa pili masaa ya asubuhi katika makao makuu ya *KENHA* yaliyoko katika eneo la Shimanzi, na *Engineer* aliweza kutambua ya kwamba wakaazi wa eneo lile hali yao ya afya ina matatizo sana kutokana na vumbi ambalo linasababishwa na ujenzi wa barabara ya Changamwe kuelekea uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Spika uongozi wa *Kenya National Highway (KENHA)* uliweza kukubali ya kwamba ni kweli uchafuzi huu umeweza kusababishia watu wa Changamwe matatizo mengi lakini wakakubali ya kwamba hatua za dharura zimeweza kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba maji yanamwagwa kwa wingi wakati kazi hii ya barabara ikiendelea.

Mheshimiwa Spika vilevile Eng Makori aliweza kukubali ya kwamba mbali na mawe yalipomwagwa katika barabara zile barabara ndogo zinapitia katika mitaa ya Changamwe zitaweza kukarabatiwa kupitia kwa *Kenya National Highway Authority* ili ziweze kuunganishwa na barabara kuu ambayo inaelekea uwanja wa kimataifa wa ndege.

Mheshimiwa Spika kama Mwenyekiti napenda kuwahakikishia wakaazi wa Kaunti ya Mombasa, hasa hasa wakaazi wa Changamwe na jamii nzima kwa jumla ya kwamba Kamati inafanya kazi na *Kenya National Highway Authority* kwa karibu na kuhakikisha ya kwamba matatizo mengi yale ambayo yanawapata wananchi kufuatia kwa ujenzi wa barabara hii kuu yataweza kutatuliwa kadri barabara hii inavyoendelea.

Mheshimiwa Spika *Engineer* alituhakikishia ya kwamba kufikia mwezi wa tano kazi hii ya ukarabati itakuwa imeweza kukamilika na matatizo haya yataweza vile vile kuweza kusitishwa baada ya ufunguzi wa barabara hii kuu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Thank you very much, yes Hon Jimmy Odari.

**Hon. Odari:** Thank you Hon Speaker. Hon Speaker I would like to state that am not satisfied with the response of the Hon Chairman for Environment because Mr. Speaker when I stood here the other day requesting for the statement from the Committee in regard to the problems that are affecting the people of Changamwe, I stated out several points, among the

points that I stood out I've just heard two responses as opposed to be several items which I stated; for example this construction and I want to emphasize that we are not opposed to development we very much, we as people of Changamwe we very much appreciate developments, the construction of new highway at Changamwe is a welcomed project and anybody will be happy to have development in their area.

However this development as much as it is good has come with a lot of problems that are affecting my people and amongst them apart from the dust which is affecting my people's health adversely, there many other things which I expected the Committee to address amongst these things is the problem of sewage.

The sewage system in Changamwe is affected Mr. Speaker, many toilets are blocked because the main sewage line is affected by the construction, streetlight for example they have had to be relocated; some of street lights were affected in that they were removed to pave way for the expansion of the road but they have never been restored up to now.

The access roads I've heard him saying that are going to be repaired let us hope that they are going to be repaired because my fear as I stated earlier is that the contractor may decide to leave the site without addressing the problem.

Another thing Mr. Speaker in this construction there are many *Jua kali* traders in my area estates whose livelihood is dependent on the little business that they are carrying out and they have been removed from their places without compensation.

Hon Speaker delayed water supply to the estates is been affected, the water which they use to receive before the inception of the project is no longer available and the people are already suffering.

So I expected the Chairman of the Enviroment Committee to come up with a very comprehensive report after having visited the Kenya National Highway Authority; I expected that they would come with a report come sit down... and compile a comprehensive report which is satisfactorily because I owe my people an explanation and they are in fact waiting for the response from this Assembly.

So Hon. Speaker I wish to ask through your Chair that the Committee go back and do a thorough job instead of coming up with shoddy answers. Thank you Hon. Speaker.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Amir Thoya.

**Hon. Thoya:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa nafikiri hili ni Nyumba la sheria na tunapotoa mwelekeo wa kazi fulani iweze kufanywa nataka kuwahakikishia kwamba ni sheria tu peke yake ndiyo ambayo inayoweza kutuongoza kuhakikisha kwamba kazi kama ile kupitia kwa kiti chako kimeweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika Mheshimiwa ambaye amezungumza sasa hivi ni Mwakilishi wa eneo la Changamwe na ndiye ambaye aliweza kuleta taarifa hii; mimi mwenyewe kama Mwenyekiti wakati nilipokuwa naenda kwenye kikao kile niliweza kuwasiliana na yeye kwa sababu kikao kilikua kimepangwa masaa ya saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Spika nilipomuita aliniambia ya kwamba ameshikika na akanitumia tu ujumbe kupitia *sms* yale mambo yanayo muathiri katika eneo lake; ikiwa kile kikao ni muhimu kiasi kwamba hata kama yeye angelikua yeye anawakilisha kwake vyema angeweza kuwacha zile shuguli ambazo zilikuwa zinafanyika wakati ule ili aje aweze kuwakilisha watu wake vyema kuliko kuniambia ya kwamba atanitumia yale matatizo ambayo yanaathiri watu wake kupitia kwa ujumbe mfupi.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi nilizungumza naye lakini masikitiko ni kwamba leo anakuja hapa kana kwamba hajui kwamba mimi na yeye tuliweza kufanya mawasiliano. Ahsante sana, Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Wangundi, what is it?

**Hon. Wangundi:** Mheshimiwa Spika nitatoa taarifa kwa Nyumba hili ya kuwa jukumu la Mheshimiwa Jimmy Odari ni kuwasilisha matatizo yanayokumba wakaazi wa eneo lake katika Jumba hili wala si kufuata mahali Kamati inaenda kufanya upekuzi na kujua chanzo na suluhu watakazo fuata yeye ya kwamba ahudhurie.

Mheshimiwa Jimmy Odari alileta matatizo yanayohusu wakaazi wa Changamwe Mheshimiwa Spika na nazungumza hivyo na mimi nikiwa mwenyeji wa Changamwe pia; kwa hakika tuko na matatizo na unapokumbuka vizuri ujenzi wa barabara ule ulicheleweshwa kwa muda fulani sababu kubwa ikiwa ni yale mashirika yanayohusika yalikuwa hayajalipwa, hivi sasa tunavyozungumza mashirika yote yamelipwa.

Mheshimiwa Spika kama ni shirika la umeme nchini, *Kenya Power* limelipwa, kama ni idara ya maji imelipwa na kila mmoja achukue jukumu lake kukaa na shirika la *KENHA* halitaleta suluhu kwa sababu wale mashirika ambao wamehusika wote washapokea fedha na kila mmoja atekeleze majukumu yake.

Kama ni kuhamisha nyaya za stima ahamishe kabla barabara haijaanza kujengwa, kama ni kuhamisha *pipe* za maji ikamilishwe kabla barabara haijaanza kujengwa, kama ni kuhamisha line ya maji taka ni maswala ambayo yanafaa yaangaliwe kwa upana yaangaziwe vikamilifu na serikali hii iwapo Kamati inachukua jukumu ya kuzingatia mambo haya yaweze kutekelezwa walete ripoti iliyokamilika.

Mheshimiwa Spika ripoti ile haijaleta suluhisho ya matatizo yanayokumba wakaazi wa Changamwe kwa ujumla, napinga ripoti ile.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon Jimmy Odari we cannot discuss the statement, it's a statement, If you are not satisfied with the response you come with a Motion, it's a statement and if not satisfied you come with a Motion to compel the people concerned to do what you want them to do. Yes Clerk?

*(Interruption)*

Mr. Speaker!

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): We are not discussing, we are not going to discuss the statement, the statement will not be discussed and we are not debating the statement we only debate a Motion.

**Hon. Mwalimu:** It's just information.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): But no debate on the statement. Yes what is it?

**Hon. Mwalimu:** Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker it is a concern I also reside from Changamwe and to add on am a Member of Transport Committee. Mr. Speaker I think some of the Honorable Members who are in that Committee will concur with me that we have not sat on this issue.

*(Applause)*

...It is an issue affecting our people Mr. Speaker and we should take it seriously. Thank you.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon Fadhili I think we have finished deliberating on this matter, Hon Mwadziwe you cannot debate a statement we only debate...

*(Interruption)*

We only debate a Motion....

*(Interruption)*

I hope you are not debating; you are not contributing to this. So what is it?

**Hon. Mwinga:** Mr. Speaker I just wanted the question from you the Chair because the one who brought the statement is talking of Environment Committee and the person who has responded is the Chairman of Roads and Infrastructure.

So we are confused Mr. Speaker is it supposed to be brought by Chairlady of Environment or was it supposed to be brought by Chairman of Transport and Infrastructure; we are confused the House is confused.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Okay thank you very much, Hon. Jimmy Odari you will compile your concerns and put them in a Motion and then you bring back to this House as a Motion compelling the appropriate authorities to amend or to do, to make good what is bad in that ward. Yes Hon Zainab?

**Hon. (Ms.) Zainab Kithinzi:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika naomba kupitia kwa kiti chako uweze kunipa ruhusa nitoe taarifa ambayo niko nayo, ni muhimu.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Zainab we have got an Order paper here; tomorrow is a statement day on Thursday afternoon, so you will bring your statement tomorrow. Yes Clerk.

### MOTION

Hon Mary.

**Hon. (Ms.) Akinyi:** Thank you Mr. Speaker Sir. Mr. Speaker Sir I wish to table a Motion on Installation of County Billboards at the County Boundaries.

*(Hon. (Ms.) Akinyi moved Motion on Installation of County Billboards at County Boundaries)*

Mr. Speaker Sir,

That AWARE THAT, the County has several entry road gateways at Shika Adabu, Shimo la Tewa, Mwakirunge and Miritini.

FURTHER AWARE that, the existing billboards welcoming visitors to the County are faint or in some cases do not exist;

CONCERNED THAT, visitors may not be aware or properly guided as to our County boundaries;

I urge this Assembly to **RESOLVE** that:

The County government to install billboards on entry roads; at County boundaries for guidance to visitors and members of the public.

*(End of motion)*

Mr. Speaker Sir I asked Hon Enock to second the Motion.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Mwakirunge.

**Hon. Mwinga:** Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker I stand here to support the Motion.

*(Interruption)*

**Hon. Wangudi:** Mr. Speaker the Hon Member has not seconded the Motion but has supported.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Can you second the Motion properly do you support or second?

**Hon. Mwinga:** Mr. Speaker I think my neighbour here Hon. Wangudi is trying to distort the statement. Mr. Speaker I said I rise here to second the Motion.

*(Laughter)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): That's nice Members I now propose a question; it is proposed that the County Billboards to be put at the County boundaries. Yes Hon Mary Akinyi.



**Hon. Akinyi:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika kama vile tujuavyo kuwa Kaunti yetu ya Mombasa iko na mipaka na Kaunti zengine, Kaunti jirani kama Kaunti ya Kwale na Kaunti ya Kilifi.

Mheshimiwa Spika kutokana na kuwa kuna Kaunti nyingi ambazo pia ni majirani zetu ningeomba Jumba hili tukubaliane kuwa tuweze kuweka ishara ya kuonyesha kuwa tuko katika Kaunti yetu ama tuko katika Kaunti ambayo ni ya jirani na hizi ishara kama zitaweza kuweka serikali yetu ya Kaunti itaweza kuweka mabango ya kuwa ishara inaonyesha kuwa tuko Mombasa ama tuko katika Kaunti nyengine ambao ni jirani. Mheshimiwa Spika nasema mambo haya kwa sababu...

*(Interruption)*

**Hon. Oduor:** Point of Order.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): What is your point of order?

**Hon. Oduor:** Actually it is a point of correction because I... *(Inaudible)*

*(Laughter)*

The Honorable Member is emulating I wish clarity because I know in America the new President is doing something like this they are building a boundary...

*(Laughter)*

So am not sure is it billboards on the roads or on all the boundaries Mr. Speaker because where my friend comes from in Mwakirunge there's a road there and does it mean even in those other areas; so is this like the Somali thing, anti terrorism or which borders.

Mr. Speaker you know please Hon Mary please clarify is it main roads or on the boundaries so that we can know if it is the billboards at the boundaries...

*(Laughter)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Mary.

**Hon. (Ms.) Akinyi:** Ahsante Mheshimiwa Spika nilikuwa bado naendelea kujenga mswada wangu lakini ni vile viingililio vya Kaunti yetu ndio ningependa tuweze kuweka ishara ya kuonyesha kuwa tuko katika Kaunti nyengine ama tuko katika Kaunti yetu ya Mombasa ili hata wageni ili wanapotoka kule nje wanataka kama kuna ishara ya bango ambayo inawakaribisha 'karibuni Mombasa' na wanapotoka Mombasa inawaambia 'Kwaherini mfike Salam Muendako'.

Mheshimiwa Spika nasema jambo hili nikiwa nawekea mkazo kwa sababu wakati mwengine mambo mengine wanaweza kupeleka mambo ambayo si mazuri yanaweza kutendeka katika Kaunti ambayo si Kaunti na hali sisi Kaunti yetu ya Mombasa ni Kaunti 001 ambapo mambo yote hata Kaunti zengine zote hata za kutoka kule nje huwa zinakuja kuigizia mambo ambayo huwa yanatendeka katika Kaunti yetu ya Mombasa ambayo ni Kaunti 001.

Hivyo basi Mheshimiwa Spika ningeomba tukubaliane kuwa serikali ya Kaunti ituwekee yale mabango ambayo yanaonyesha kuwa hii ni Kaunti ya Mombasa wakati wanapoingililia, hii ni Kaunti ya Kwale, ile ni Kaunti ya Mombasa, ile ni Kaunti ya Kilifi katika hizo sehemu zilizoko ama zimepakana na Kaunti yetu ya Mombasa.

Naomba Nyumba hii munisaidie kuunga mkono mswada huu mzuri ambao tutaweza kuboresha Kaunti yetu ya 001, imeendelea katika maendeleo yote. Ahsante.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Zainab Kithinzi.

**Hon. (Ms.) Zainab Kithinzi:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii. Mheshimiwa Spika nimesimama hapa kupinga kabisa mswada huu...

*(Applause)*

Mheshimiwa Spika nafikiri mwenzetu Mheshimiwa Mary Akinyi ningemuomba atembe kwa sababu ikiwa unaelekea upande wa Ukunda ukivuka *ferry* kuna mahali kunaitwa

*Check Point* kwenye mpaka wa Kwale na Mombasa kuna *check point* pale ya kuonyesha kuwa huku ni Mombasa na huku ni Kwale.

Ukielekea upande wa kilifi ukifika Mtwapa, Mtwapa pale utakuta kuna bango linasema huku ni Mombasa na huku ni Kilifi, hali kadhalika ukiendelea upande wa barabara ya Nairobi ukifika Miritini nataka kushika Mazeras kuna bango pale linaonyesha pale Mheshimiwa Spika,

Kwa hivyo kama tutatengeza mabango mengine huko ni kuharibu pesa au nikufuja pesa za umma na hizo kazi hizo zinaweza kufanya tunaweza tukaziongeza mahali zikatusaidia lakini ikiwa ni zile viashirio zinazoonyesha ziko; ningemuomba aweze kutembea ili aweze kuwa sawa Mheshimiwa Spika. Ahsante.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Saad Faraj.

**Hon. Faraj:** Thank you very much Mr. Speaker for this opportunity. Mr. Speaker I think this House should prioritize issues and as a matter of priority we should be discussing today in this House issues regarding to hunger and those areas which are being affected and other sectors like that which are currently in the doldrums and these are issues that we need to come up with.

I stand Mr. Speaker to oppose this Motion and I oppose because first Mr. Speaker these are the departmental issues; these issues should be discussed at departmental level between the CECs and the Section heads of that particular department.

I am sure very clearly we are running out of issues, such kinds of Motions so Mr. Speaker mine is to say that these are issues which should be discussed at the departmental level and not this level. Thank you very much Mr. Speaker.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Stephen Wangudi.

**Hon. Wangudi:** Mheshimiwa Spika nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa...

*(Applause)*

...Kwa kuwasilisha mswada mzuri sana katika Nyumba hii lakini Mheshimiwa Spika bila kupoteza muda moja kwa moja nitaenda na niko na hoja za kutosha za kupinga mswada huu....

*(Applause)*

...Mheshimiwa Spika ninaomba kupinga mswada huu kwa sababu zilizoko; wakaazi wa Mombasa wanajua mpaka wao, wakaazi wa Kwale wanajua mpaka wao, hatuna haja ya kuwakumbusha iwapo kuna wageni, kuna watalii huwa kuna wale wenyeji wanaowaelekeza.

Hatuna haja Mheshimiwa Spika kuharibu pesa zetu, nimekosa bahati ninawakilisha wodi ambayo imezingirwa na mitaa ya maji Mheshimiwa, kila mara husema hivi sasa tunavyozungumza kutoka mtaa wa Mathare kuvuka kama mita 20 inachukua kutembea mita 200 kwa dakika 20, kisa maana hakuna daraja la kuvuka na miguu. Daraja ambalo linaweza kujegwa na chini ya nusu milioni halijafanyika mpaka hivi sasa.

Tumechukua jukumu la kuleta wahandisi mara saba, Mheshimiwa Spika hivi sasa niunge mswada aidha utatumia pesa na ambao hauna manufaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika lakini tunaleta katika Mombasa tuko na uhaba wa maji sina hata kisima kimoja kimechimbwa na serikali ya Kaunti, kile kimechimbwa wakati ule hakitoi maji, badala ya kutuletea Mswada Mheshimiwa ya kuleta kuweza kuchimba visima katika mashule yetu na katika mitaa yetu tunaweka mabango...

*(Interuption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes what is it Hon Saad Faraj.

**Hon. Faraj:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nilikuwa na tashwishi kidogo kwa ndugu yangu Mheshimiwa Wangudi kwa kuwa anadhalilika kuwa sisi hatukuleta Mswada kama huo yaani sijui alikuwa wapi kwa miaka minne asilete Mswada hiyo ili tuweze kusaidia watu wake.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Wangudi.

**Hon. Wangudi:** Mheshimiwa Spika nimesema nimeweza kutengeza mazingira zaidi ya mara tano, zaidi ya mambo ambayo watu wanahangaika.

Tatizo linalokuja ni hakuna kitu Mheshimiwa Spika, hilo ni swala ambalo linajitokeza iwapo kuwa hakutakuwa leo hii tuwekeni mabango katika Kaunti yetu, kwa sababu hayawezi kuongeza jambo lolole katika maisha ya wakaazi tunaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika ninaomba wenzangu tupinge Mswada huu ili kesho tupate Mswada mbadala wa huu wa kuleta maendeleo...

*(Applause)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Amur Mufad.

**Hon. Amur:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika ni masikitiko kwamba Waheshimiwa wengine mpaka leo hawajaelewa ya kwamba kutaka kufanya jambo lolote mpaka uwe umekuwa *factored* katika bajeti; leo twazungumzia kwenda kujenga mabango, bango moja Mheshimiwa kwa uchache ninavyoelewa mimi sio chini ya nusu milioni, twende tujenge mabango mangapi? Hajatuambia Mheshimiwa ni ngapi? Pili saa hii sisi tunakabiliwa na shida ambayo ni muhimu sana...

*(Interuption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Hatimy, What is it?

**Hon. Mohamed Hatimy:** Mheshimiwa Spika nafikiri *order* 44 iko wazi mtu yeyote Mwanachama wa Kamati ana haki ya kuja na Mswada wakati wowote ile anaona ni sawa, kwa hivyo...

*(Applause)*

Waheshimiwa kuwa walete Mswada mwingine ambao Mheshimiwa Spika haiwezekani, ni haki yake kuleta Mswada na ni lazima asifukuzwe ikiwa muktaka kupinga pingeni lakini lazima apewe nafasi yake mimi naunga mkono...

*(Laughter)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Murfad?

**Hon. Amur:** Mheshimiwa Spika serikali ya Mombasa au Kaunti ya Mombasa hawakuweza kufanya jambo lolote, lazima kwanza kuwe kumetengwa kitita cha pesa cha kufanya jambo lile, sisi jambo hili halijakuwa *captured* katika bajeti yetu leo vipi sisi tutaenda kuweka kitu ambacho hakiko kwenye matumizi ya bajeti ya Mombasa?

*(Interruption)*

**Hon. (Ms) Akinyi:** Point of Information!

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Mary Akinyi.

**Hon. (Ms) Akinyi:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Ningependa kufahamisha Jumba hili kuwa wakati huu ndio sasa tunaenda kwa bajeti ndio tunaenda kwa bajeti yeye anajuaje kama hiyo...ninajua hii iko katika bajeti kwa sababu nimeileta.

Kwa hivyo asituambie kuwa haiko kwa bajeti na bajeti hatujasoma na ndio tunaelekea kwenda kusoma bajeti. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Amur can you continue.

**Hon. Amur:** Mheshimiwa Spika ni masikitiko kwamba ndugu yangu aliyezungumza dakika chache zilizopita hakuwa hakuenda Jumatatu kupitia *Fiscal Strategy Paper* ambayo ilikuwa imekusanya mkusanyiko wa bajeti, ni masikitiko wakati haijakuwa *captured* sasa itakuwa vipi?

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon Hatimy what is it?

**Hon. Mohamed Hatimy:** Mheshimiwa Spika nafikiri jana tulisema kuwa kuna *supplementary budget*....

*(Applause and laughter)*



Wengine wana *influence* kwa hiyo watapambana.....

(*Laughter*)

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Amur.

**Hon. Amur:** Mr. Speaker it was clear in the supplementary budget there were only two items; the grant for the bursaries and for the health, so for any other issue its either it should be proposed in written to the Committee concerned so that it can be captured other than that nothing that has been allocated funds can be implemented in this County.

Mr. Speaker two, that IEBC had determined the boundaries of 47 Counties in this country, each boundary of this 47 County...

(*Laughter*)

...I want to know for us to be told someone doesn't know his boundaries it is unlike him or her, thank you Mr. Speaker.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Mwadziwe.

**Hon. Mwinga:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika nimesimama hapa kuunga mkono Mswada wote.....

(*Applause*)

Mheshimiwa Spika nafikiri wote Waheshimiwa walioko ndani Nyumba hii wanajua mimi natoka Mwakirunge na pale Mwakirunge ni mahali ambapo pamekaa huwezi tofautisha Kilifi ni wapi na Mombasa ni wapi na ndio maana nimekuja nikaongea katika Nyumba hii nikasema kuna mambo yanafanyika kule Kilifi na watu wanafikiria labda haya mambo ni ya Kaunti ya Mombasa.

Mheshimiwa Spika lakini yale mambo yanayofanyika hayakuwa yetu yalikuwa upande wa pili, kwa hiyo kupitia kwa Nyumba hii nataka kueleza Waheshimiwa wenzangu ya kwamba kama hizi, kama haya mabango ambayo yanawekwa katika zile barabara kuu lakini kuna zile barabara zengine ndogo ndogo kama ile yangu ya Mwakirunge ni ya mchanga ile ni barabara ambayo saa hii inapitisha hata watalii.

Kwa hiyo Mheshimiwa Spika nakuomba ni kwamba sio ati tunataka kutengeneza mabango ya ma *entrance*...

(*Interruption*)

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Wangudi what is it?

**Hon. Wangudi:** I just want to know if we are constructing billboards.....

(*Laughter*)

But it's better to struggle for the construction and improvement of Mwakirunge road than putting the billboards Mr. Speaker, thank you.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Honorable of Mwakirunge can you continue.

**Hon. Mwinga:** Kwa hiyo Mheshimiwa Spika nilikuwa nataka kuelezea Nyumba hii ni ya kwamba hata yale ambayo yamewekwa katika zile barabara kubwa sio mabango ya pesa nyingi.

Mheshimiwa Spika pale Mwakirunge tungewekewa mabango hata kama ni sita kwa sita ile tu kuonyesha ya kwamba sasa umeingia upande wa Kaunti ya Mombasa umeacha Kaunti ya Kilifi umeingia Kaunti ya Mombasa, nafikiri jambo la...

(*Interruption*)

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon Hatimy what is it?

**Hon. Mohamed Hatimy:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa anayeongea....angei *second the motion* badala ya kuirudilia tena mara ya pili.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Ok it has been seconded by the head you can continue, yeah by nodding I saw you seconded by nodding; yes you can continue Hon. Mwadziwe.

**Hon. Mwinga:** Ahsante Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Spika mimi nikimalizia ninaomba Waheshimiwa tukubaliane ya kwamba hata yale mabango ambayo ninasema yamevekwa yamefutika kama ile ya pale Mazeras ile imefutika kabisa hata haionekani.

Kwa hiyo Mheshimiwa Spika kama sio kutengeneza hizo mpya lakini hata zile ambazo ziko zinatakikana zirekebishwe ndio angalau watu waweze kujua wameingia katika Kaunti ya Mombasa...

*(Interruption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon Kithinzi what is it?

**Hon. (Ms) Zainab Kithinzi:** Mheshimiwa Spika ningependa kufahamisha hii Nyumba ya kuwa hata Mheshimiwa mwenye ameongea kwake mwenyewe Mwakirunge iko na haijui kama iko ama haiko, sielewi Mheshimiwa huyu yuwatembea ama hatembei, ya Mazera iko haijafutika, ya Mwakirunge iko katikati ya Mwakirunge na Kilifi ndio sababu watu wavukishwa huelewi uko wapi wapi hujielewi kwa ufupi ahsante Mheshimiwa Spika...

*(Laughter)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon. Mwadziwe?

**Hon Mwinga:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa aliyetoka kuongea si makosa yake, ni kwa sababu nilimtafutia ploti kubwa kule Mwakirunge sasa anajaribu kukueleza kuonyesha yeye anajua kuliko mimi lakini yeye hajui tukikupatia ka ploti pahali hapo hapo mbali sana na ule mpaka anaosema...

*(Laughter)*

Mheshimiwa nafikiri namalizia na kusema Mheshimiwa Spika Mswada huu Mheshimiwa Spika ni mzuri na zile bango ziweze kupakwa rangi zichorwe vizuri ili wageni wote wanao kuja Kaunti ya Mombasa waweze kujua sasa wameingia Mombasa Kaunti 001. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Fadhili.

**Hon. Mwalimu:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwanza nasimama nikitangaza msimamo wangu kwanza kwa hoja hii. Mheshimiwa Spika ni kazi ambayo najua iko mbele yake na mimi niko na *interest* na kazi hii, mimi naunga mkono hoja hii.....

*(Laughter and applause)*

Ndio maana nimesimama nika *declare interest* yangu Mheshimiwa Spika twaelewa kuwa mapambo ni muhimu kila mtu anapendelea mahali pawe pazuri pa kuridhisha, pa kuvutia, pa kupendeza; ikiwa tutaweka Kaunti yetu katika hali ya kupendeza, hali ya kuvutia itakuwa ni vizuri zaidi na mimi namuunga mkono Mheshimiwa aliyelea hoja hii tena wakati huu kwa sababu kama alivyozungumza Mheshimiwa mmoja aliyetangulia kwamba kuna shughuli za wengine zinafanyika maeneo ambayo si ya Mombasa lakini inasemekana ni ya Mombasa, kwa sababu gani, hakuna sehemu itakuonesha hapa si Mombasa.

Sasa kuna mabaya ambayo yanatokea hayatokei katika Kaunti yetu lakini twabandikizwa kuwa ni Mombasa Mheshimiwa Spika, tunaona Kaunti zengine mpaka leo miaka minne tangu Kaunti zianze kufanya kazi watu bado wanazozana kuhusu mipaka na hapa hapa ndani ya Bunge hili wako Waheshimiwa hawajui mipaka yao ya wodi yao.

Sasa Mheshimiwa Spika mimi naona iko haja tena kubwa ya kuweza kuelimisha Waheshimiwa mipaka yao....

*(Laughter)*

Ya wodi, mimi nashangaa ukiona Mheshimiwa wa Shanzu anaenda mpaka Mwakirunge, mimi nashangaa ukiona Mheshimiwa wa Tononoka anaenda mpaka maeneo ya Mikindani mimi nashangaa....

*(Laughter)*

...Mheshimiwa Spika hoja aliyoleta Mheshimiwa wetu mimi naona ni hoja nzuri; kwanza tujue wodi zetu alafu natujue Mombasa yetu yaanzia wapi na yamalizikia wapi kando na zile ambazo zipo, maana kuna Mheshimiwa mmoja amesema zipo lakini tunaomba ziongezeke maana ikiwa zimewekwa katika hizi barabara kubwa za kupita magari kuna sehemu zingine hakupiti magari lakini ni sehemu zetu, na tukijiweka sawa hata ikiwezekana kama alivyozungumza Mheshimiwa mmoja ametupatia mfano wa Amerika kuwa kunajengwa ukuta ikiwa twaweza tufanye hakuna shida kama pesa tunazo lakini kama basi tujipange tuweke Kaunti yetu katika hali ambayo mtu akifika ajue hapa yuko katika kijiji fulani, niko Mombasa, niko sehemu fulani.

Maana kuna vijiji vingine hata hatu vitambui na barabara zingine zimepita huko ndani ndani ukiwa unatokea Nairobi unakuja Mombasa zamani wakati wa Manispaa ile mipaka ilikuwa karibu kilomita mbili mbele lakini hivi sasa hivi tunavyo itambua imerudishwa nyuma na mimi naona iko haja kubwa sana tujue mipaka yetu na tutatue hili tatizo na mapema kabla kizazi kijacho kije kipate shida.

Kama tunavyo ona Makadema, Taita Taveta na Kwale bado wanazozana katika mipaka unashindwa mmoja bado wanapigania na si Kaunti hizi mbili peke yake Kaunti nyingi sana Kenya hii bado wanazozana katika mipaka.

Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi nawaomba wenzangu waunge mkono hoja hii kwa sababu ya ile sababu niliyoiweka pale mwanzo ambayo nilitangaza *interest* yangu najua ikipatikana na sisi tutaweza kusonga mbele. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Thank you very much for the absence of further debate I will leave to Hon Mary who moved the Motion to reply to the Motion. Hon. Mary Akinyi?

**Hon. (Ms) Akinyi:** Ahsante sana Mheshimiwa spika ningependa kushukuru walioniunga mkona kwa mjadala huu na hata wale wamepinga pia nawashukru pia sababu ni mambo yao vile wanavyotaka Mheshimiwa spika ningependa kupitia kwako niende nikafanye marekebisho kidogo...

*(Applause)*

...ili tuweze kuzungumza na shirika la pema wakati wanapotengeneza zile barabara vile wanavyo eka alama alama zako vile hakuna pesa ili wanapotengeneza barabara zao waweze kutuwekea alama za kuonyesha za kuingia Mombasa, hapa ni Kwale ama ni wapi, ahsante Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Thank very much Hon Mary Akinyi I think this Motion will come back in amended form. Yes Clerk.

#### **ADJOURNMENT**

Members let there be no other business the House stand adjourned till tomorrow in afternoon. Thank you.

The House rose at 3:53pm.